# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

## SHULE YA SEKONDARI IGUNGA

### MAELKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IGUNGA-2024

PICTURE

**Mawasiliano**

**Mkuu wa Shule:0784905605**

**Makamu Mkuu wa Shule : 0710931999 au 0755464935**

**Matroni: 0756650854**

**Patroni:0693523160/0717658997**

**Shule ya Sekondari Igunga**

**S.L.P.169,**

**IGUNGA**

**Tarehe 24/4/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IGUNGA HALMASHAURI YA IGUNGA MKOA TABORA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari Igunga mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya **HKL/ HGE/ HGK/ HGLi/ HGFa**

Shuleya Sekondari Igunga ipo umbali wa nusu Kilometa Kaskazini mwa Mji wa IgungaUsafiri wa **bodaboda/bajaji** kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi ya Igunga Nauli ni Shilingi 1000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01,Julai,2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01,Julai, 2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **01,Agusti,2024.**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.0 Sare za Shule**

**i.** Sare ya shule hii ni **kijani nyeusi(dark green)**.kwaWasichana –(Ashone) Sketi mbili za linda boksi kubwa mbele na nyuma madogo mawili za urefu wa kufika kwenye vifundo vya miguu isiyo bana (na **kijani nyeusi (dark green)** kwa Wavulana

**ii.** Mashati mawili (2) rangi nyeupe mikono mirefu au nusu kanzu ifike mapajani na mikono ifike kwenye vifundo.

**iii.** Rangi ya Juba ni nyeupe na lifunike mpaka kwenye vifundo vya mkono.

**iv.** Sare ya Michezo ni T-Shirti nyekundu yenye kolla Kwa wasichana na T-Shirti nyekundu yenye kollakwa wavulana.

**v.** Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

**vi.** Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana nanyeusi kwa wavulana.

**vii.** Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

**viii.** Sweta la kijani jeshi

**ix.** Nguo za kushindia (*shamba dress*) t-shirti za njano (yenye nembo ya shule ya Igunga sekondari) kwa wavulana na wasichana na sketi za light blue kwa wasichana na suruali za light blue kwa **wavulana.**

**x.** Tai rangi ya kijani jeshi

**xi.** Track suti ya blue bahari kwa wavulana na wasichana.

**2.1.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 counterbook kuanzia quare 2
ii. **Ream (A4)** mbili ( double A) kwa mwaka;
iii. Scientific Calculator; kwa wanafunzi wanaosoma **HGE**
iv. Godoro size ya(2x6)
v. Shuka 2 ( blue bahari na pinki), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1;

vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini, reki 1, panga 1, mifagio 2(HARD NA SOFT BROOM , MOPPER 1.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**2.1 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina yaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Kwa mwanafunzi asiyekuwa na bima ya afya atatakiwa kulipia fedha ya bima ya afya Tshs 50,400/= vinginevyo hatapokelewa.**

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule : **50901100025** IGUNGA SECONDARY SCHOOL(NMB)

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla nijambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

## 3.2 Makosa ya takayo sababisha Mwanafunz ikufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wotewawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywajiwa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulalawageni;
**xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;**

xvi. Kudharau Bendera yaTaifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na FomuMuhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Pichanne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Jina la Mkuu wa Shule :LEONATUS BUSWELU**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IGUNGA
S.L.P. 169
IGUNGA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0784905605**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0710931999/0755464935**
- **MwandamiziTaaluma: 0624784643**
- **MwandamiziMalezi :0710931999**

PICTURE

**FOMU NA.1**

**IGUNGA SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all FORM – entrants

Please examine the under mentioned student as to his/her physical and mental fitness for his/her full time student of the school.

Student's name: ………………………………………………………………………………………

Age:

……………………………………………………………………………………………………………

Blood found (red and white): ……………………………………………………………………

Stool examination: ………………………………………………………………………………

Urinalysis: ………………………………………………………………………………………

Venereal: ……………………………………………………………………………………………….

Disease / esc:……………………………………………………………………………………..…

TBTest: ……………………………………………………………………………………………

Eye Test: ………………………………………………………………………………………………..

Spleen: ………………………………………………………………………………………………..

Abdomen: ……………………………………………………………………………………………….

Urine for pregnant: ……………………………………………………………………………..

**ABNORMAL INFORMATION** (If any) eg. Physical defects impairment(s) eg. Arm, legs etc. infection chronic or family disease etc………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to peruse his/her education as stated above.

Signature: ……………………………………………….

Designation: …………………………………………….

Station: ……………………..…………………………

Date: …………..………………………………………

PICHA YA MWANAFUNZI

**FOMU NA.2**

**SHULE YA SEKONDARI IGUNGA**

**S.L.P 169, IGUNGA**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi: ……………………………..…………………………………………
2. Kabila……………………………………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………….
4. Alizaliwa katikaWilayaya ………………………………………………………………
5. Dini ……………………………………………………………………………………………...
6. Jina la mzazi / mlezi ………………………………………………………………………..
7. Anuani kamili yamzazi / mlezi

   **Mtaawa …………………………………………………..…**

   **Kijiji cha …………………………………………………**

   **Tarafa ……………………………………………..………**

   **Wilaya ………………………………………..…………..**

   **Mkoa …………………………………………..………….**

   **S.L.P ……………………………………………..………..**

8. Namba ya simu ……………………………………………………………………………….
9. Kazi ya mzazi / mlezi ………………………………………………………………………..
10. Taja au eleza juu ya mwanafunzi kama ana ugonjwa wowote unaohitaji uangalizi ………………………..……………………………………………………..
11. Taja udhaifu wowote wa mwili au afya alionao mwanafunzi na Uambatanishe cheti cha Daktari anayetambulika

………………..…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

….…………………………………………………………………………………………….

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

**FOMU NA.3**

**SHULE YA SEKONDARI IGUNGA**

**S.L.P 169, IGUNGA**

**AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE (MWANAFUNZI na MZAZI/MLEZI)**

Mimi ……………………………………………
Naahidi kufuata sheria, kanunina taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakapokuwa ndani na nje ya shule.
**Sitajihusisha** na migomo, fujo, wala makosa ya jinai.

Saini……………………………….. Tarehe…………………….

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………….. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ...........................................................wa S.L.P .........................**Mj**i..........................**Simu**...................................aliyeweka ahadi hapo juu, naahidi kumpatia michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

**Saini** …………………………………… **Tarehe** …………………………

**FOMU YA PICHA NNE**

Fomu ya picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni.

| | **MZAZI** | | **MLEZI** | |
|---|---|---|---|---|
| **PICHA** | | | | |

## VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAVYO

### KISWAHILI

1. KIMBUNGA
2. CHUNGU TAMU
3. MAPENZI BORA
4. VUTA N'KUVUTE
5. KUFIKIRIKA
6. MFADHILI
7. USIKU UTAKAPOKUCHA
8. MORANI
9. KIVULI KINAISHI
10. NGUZO MAMA
11. KWENYE UKINGO WA THIM

### ENGLISH LANGUAGE

1. English for A level practical approach
2. English language for A level 5&6
3. An enemy of the people
4. I will Marry I want
5. The beautiful one are not yet born
6. A man of the people
7. Betrayal in the city

### GENERAL STUDIES

1. Understanding advanced level general studies
2. General studies Notes

### HISTORY

1. Major in Africa History
2. Major events in African History
3. The political economy and imperialism
4. Africa since 1800-4$^{th}$ edition
5. The 20$^{th}$ CENTURY
6. Europe from 1815

### GEOGRAPHY

1. Regional geography
2. General geography in diagrams
3. Certificate human and economic geography